TANGAZO LA SERIKALI NA. 693 la tarehe 02 /12/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA SITALIKE YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Sitalike ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na wa kina wa eneo

3. Mpango wa jumla na wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji P1 yenye majira ya nukta 297771.957E, 9270000.000N inayopatikana Mto Kabenga; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa S 64º 33' 43" W hadi alama ya mpaka ya upimaji P2 yenye majira ya nukta 294615.234E, 9268612.948N kwa umbali wa kilomita 0.527; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa S 15º 56' 14" E hadi alama ya mpaka ya upimaji P3 yenye majira ya nukta 294689.714E, 9268352.127N kwa umbali wa kilomita 0.271; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa S76º 15' 22" W hadi alama ya mpaka ya upimaji P4 yenye majira ya nukta 294340.297E, 9268266.666N kwa umbali wa kilomita 0.359; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa N 15º 37' 17" W hadi alama ya mpaka ya upimaji P5 yenye majira ya nukta 294313.288E, 9268363.261N kwa umbali wa

kilomita 0.100; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa S 65º 17' 29" W ukikatiza Barabara ya Mpanda/Sumbawanga hadi alama ya mpaka ya upimaji P6 kwa umbali wa kilomita 2.287; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki ukikatiza Mto Katuma katika uelekeo wa S 72º 07' 22" E hadi alama ya mpaka ya upimaji P7 inayopatikana Darajani yenye majira ya nukta 294715.00E, 9266731.000N kwa umbali wa kilomita 2.655; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini sambamba na Mpaka wa Mbuga ya Taifa ya Katavi katika uelekeo wa S 04º 47' 31" W hadi alama ya mpaka ya upimaji WK 60 yenye majira ya nukta 294182.000E, 9260373.000N kwa umbali wa kilomita 6.380; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki sambamba na Mpaka wa Mbuga ya Taifa ya Katavi katika uelekeo wa N 88º 30' 01" E hadi alama ya mpaka ya upimaji WK 45 katika Barabara ya Mpanda – Mpimbwe yenye majira ya nukta 308277.000E, 9260742.000N kwa umbali wa kilomita 14.099; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini –

Magharibi katika uelekeo wa N 19º 56' 05" W hadi alama ya mpaka ya upimaji WK 301 yenye majira ya nukta 307070.000E, 9264070.000N kwa umbali wa kilomita 3.540 sambamba na Barabara ya Mpanda – Mpimbwe na Msitu wa Hifadhi Msaginia; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa N 74º 41' 50" W hadi alama ya mpaka ya upimaji WL 655 yenye majira ya nukta 298423.000E, 9266436.000N kwa umbali wa kilomita 8.964 sambamba na Msitu wa Hifadhi Msaginia; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa N 10º 21' 08" W hadi alama ya mpaka ya upimaji P1 yenye majira ya nukta 297771.957E, 9270000.000N kwa umbali kilomita 3.621, ulipoanzia".

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*